

**KUMB: PPR/17 - 2/1**

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA**  
**JUMATANO, TAREHE 1 FEBRUARI 2017**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 1 Februari 2017**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli kwa nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya aina zote yaani Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepanda ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 4 Januari 2017. Kwa Mwezi Februari 2017, bei za rejareja zimepanda kama ifuatavyo; Petroli Sh 69/lita sawa na asilimia 3.64, Dizeli Sh129/lita sawa na asilimia 7.47 na Mafuta ya Taa Sh 151/lita, sawa na asilimia 8.90, sawia. Aidha, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita bei za jumla nazo pia zimepanda kama ifuatavyo; Petroli Sh 69/lita sawa na asilimia 3.86, Dizeli Sh 129/lita sawa na asilimia 7.96 na Mafuta ya Taa Sh151/lita sawa na asilimia 9.50, sawia. Kwa kiasi kikubwa, mabadiliko haya ya bei za mafuta katika soko letu la ndani yametokana na kupanda kwa bei za mafuta katika soko la dunia, kuongezeka kwa gharama za usafirishaji (*premium*), pamoja na kushuka kwa thamani ya Shilingi dhidi ya dola ya Marekani, sarafu ambayo hutumika kununulia mafuta.
- (b) Hakutakuwa na mabadiliko ya bei za mafuta kwa mkoa wa Tanga, hii ni kutokana na kutopokewa mzigopya wa mafuta kwenye bandari ya Tanga kwa mwezi wa Januari 2017. Hivyo bei za mkoa wa Tanga kwa mwezi wa Februari 2017 zitaendelea kuwa kama zilivyokuwa mwezi wa Januari 2017.
- (c) Mamlaka inapenda kuujulisha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana vile vile kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba **\*152\*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (d) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (e) **Kampuni za mafuta zipo huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hiso ziwe chini ya bei kikomo (price cap)** kama ilivyokokotolewa na *fomula* iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 70/2016 la Mwezi Februari 2016**.
- (f) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta

katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei ndogo zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja.** Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.

- (g) Wanunuzi wanashauriwa kuhakikisha kuwa wanapata stakabadhi ya malipo inayoonesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hiyo ya malipo itatumika kama kidhibiti cha mnunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya ama kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo; ama endapo utakuwa umeuziwa mafuta yenyе kiwango cha ubora kisichofaa.

#### A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Sh/Lita)	Dizeli (Sh/lita)	Mafuta Ya Taa (Sh/Lita)
<b>Dar es Salaam</b>	1,959	1,861	1,852
<b>Arusha</b>	2,043	1,945	1,936
Arumeru (Usa West)	2,043	1,945	1,936
Karatu	2,061	1,964	1,954
Monduli	2,048	1,951	1,941
Monduli-Makuyuni	2,053	1,955	1,946
<b>Ngorongoro (Loliondo)</b>	2,134	2,037	2,027
Kibaha	1,963	1,866	1,856
Bagamoyo	1,970	1,872	1,863
Kisarawe	1,966	1,868	1,859
Mkuranga	1,968	1,871	1,861
<b>Rufiji</b>	1,986	1,889	1,879
Dodoma	2,017	1,920	1,910
Bahi	2,025	1,927	1,918
Chemba	2,044	1,946	1,937
Kondoa	2,050	1,953	1,943
Kongwa	2,014	1,917	1,907
<b>Mpwapwa</b>	2,018	1,921	1,911
Iringa	2,023	1,925	1,916
Kilolo	2,027	1,930	1,920
<b>Mufindi (Mafinga)</b>	2,033	1,935	1,926
Njombe	2,051	1,953	1,944
Ludewa	2,089	1,991	1,982
Makete	2,082	1,984	1,975
<b>Wanging'ombe (Igwachanya)</b>	2,049	1,951	1,942
Bukoba	2,174	2,076	2,067
Biharamulo	2,148	2,051	2,041
Karagwe (Kayanga)	2,190	2,093	2,083

Kyerwa (Ruberwa)	2,196	2,098	2,089
Muleba	2,174	2,076	2,067
Ngara	2,139	2,042	2,032
<b>Misenyi</b>	2,182	2,085	2,075
Geita	2,124	2,026	2,017
Bukombe	2,113	2,015	2,006
Chato	2,145	2,047	2,038
Mbogwe	2,162	2,064	2,055
<b>Nyang'hwale</b>	2,139	2,041	2,032
Kigoma	2,189	2,092	2,082
Uvinza (Lugufu)	2,202	2,104	2,095
Buhigwe	2,179	2,081	2,072
Kakonko	2,147	2,049	2,040
Kasulu	2,175	2,078	2,068
<b>Kibondo</b>	2,154	2,056	2,047
Moshi	2,032	1,935	1,925
Hai (Bomang'ombe)	2,035	1,938	1,928
Mwanga	2,025	1,928	1,918
Rombo (Mkuu)	2,053	1,956	1,946
Same	2,018	1,921	1,912
<b>Siha (Sanya Juu)</b>	2,039	1,941	1,932
Lindi	2,017	1,920	1,910
Lindi-Mtama	2,035	1,938	1,928
Kilwa Masoko	1,992	1,895	1,885
Liwale	2,038	1,941	1,931
<b>Nachingwea</b>	2,046	1,949	1,939
Ruangwa	2,048	1,951	1,941
Babati	2,081	1,983	1,974
Hanang (Katesh)	2,091	1,994	1,984
Kiteto (Kibaya)	2,092	1,994	1,985
<b>Mbulu</b>	2,093	1,996	1,986
Simanjiro (Orkasumet)	2,113	2,015	2,006
Musoma	2,137	2,039	2,030
Musoma Vijijini (Busekela)	2,177	2,080	2,070
Rorya (Ingirijuu)	2,146	2,048	2,039
Rorya (Shirati)	2,180	2,083	2,073
<b>Bunda</b>	2,128	2,031	2,021
Butiama	2,134	2,036	2,027
Serengeti (Mugumu)	2,182	2,085	2,075
Tarime	2,148	2,050	2,041
Mbeya	2,065	1,968	1,958
Chunya	2,075	1,978	1,968
Chunya (Makongolosi)	2,089	1,992	1,982
Ileje	2,079	1,981	1,972

<b>Kyela</b>	2,081	1,984	1,974
Mbarali (Rujewa)	2,050	1,952	1,943
Mbozi (Vwawa)	2,075	1,977	1,968
Momba (Chitete)	2,084	1,986	1,977
Rungwe (Tukuyu)	2,074	1,977	1,967
Morogoro	1,984	1,886	1,877
Mikumi	1,999	1,902	1,892
Kilombero (Ifakara)	2,021	1,924	1,914
<b>Kilombero (Mlimba)</b>	2,044	1,946	1,937
Kilombero (Mngeta)	2,033	1,936	1,926
Ulanga (Mahenge)	2,032	1,935	1,925
Malinyi	2,042	1,945	1,935
Kilosa	2,002	1,905	1,895
<b>Gairo</b>	2,002	1,905	1,895
Mvomero (Wami Sokoine)	1,994	1,897	1,887
Turian	2,009	1,911	1,902
Mtwara	2,031	1,934	1,924
Nanyumbu (Mangaka)	2,080	1,982	1,973
Masasi	2,056	1,959	1,949
<b>Newala</b>	2,063	1,966	1,956
Tandahimba	2,056	1,959	1,949
Mwanza	2,108	2,011	2,001
<b>Kwimba</b>	2,144	2,047	2,037
Magu	2,116	2,019	2,009
<b>Misungwi</b>	2,114	2,017	2,007
Sengerema	2,141	2,043	2,034
Ukerewe	2,168	2,070	2,061
Sumbawanga	2,131	2,034	2,024
Kalambo (Matai)	2,124	2,026	2,017
<b>Nkasi (Namanyele)</b>	2,145	2,047	2,038
Katavi (Mpanda)	2,166	2,069	2,059
Mlele (Inyonga)	2,144	2,047	2,037
<b>Songea</b>	2,082	1,984	1,975
Mbinga	2,115	2,018	2,008
Namtumbo	2,111	2,014	2,004
Nyasa (Mbamba Bay)	2,118	2,020	2,011
Tunduru	2,141	2,043	2,034
<b>Shinyanga</b>	2,087	1,990	1,980
Kahama	2,101	2,004	1,994
Kishapu	2,116	2,018	2,009
Simiyu (Bariadi)	2,129	2,031	2,022
Busega (Nyashimo)	2,122	2,024	2,015
<b>Itilima (Lagangabilili)</b>	2,132	2,034	2,025
Maswa	2,120	2,023	2,013

Meatu (Mwanhuzi)	2,127	2,030	2,020
Singida	2,049	1,952	1,942
Iramba	2,061	1,964	1,954
Manyoni	2,034	1,936	1,927
Ikungi	2,045	1,947	1,938
<b>Mkalama (Nduguti)</b>	<b>2,074</b>	<b>1,976</b>	<b>1,967</b>
Tabora	2,112	2,015	2,005
Igunga	2,066	1,969	1,959
Kaliua	2,131	2,033	2,024
Ulyankulu	2,125	2,027	2,018
Nzega	2,077	1,980	1,970
Sikonge	2,124	2,027	2,017
Urambo	2,126	2,028	2,019
Tanga	1,854	1,705	1,656
Handeni	1,875	1,725	1,677
Kilindi	1,890	1,740	1,692
Korogwe	1,866	1,717	1,669
Lushoto	1,876	1,726	1,678
Mkinga (Maramba)	1,861	1,712	1,663
Muheza	1,859	1,709	1,661
Pangani	1,861	1,711	1,663

### B: BEI ZA JUMLA

Wholesale Prices- DSM	Petrol (TZS/Lt)	Diesel (TZS/Lt)	Kerosene (TZS/Lt)
Cap Prices	1,850.56	1,753.35	1,743.59

Bei za Jumla-TANGA	Petroli (Sh/L)	Dizeli (Sh/L)	Mafuta ya Taa (Sh/L)
Bei Kikomo	1,746.22	1,596.65	1,548.48

Felix Ngamlagosi

**MKURUGENZI MKUU  
EWURA**